**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA

IMEIDHINISHWA KWA KIWANGO CHA ISO 9001:2015

TCAA

## TAARIFA KWA UMMA

## KUTANGAZWA KWA KANUNI ZA USAFIRI WA ANGA GAZETI LA SERIKALI NA. 258–268 YA TAREHE 18 SEPTEMBA 2026

Mamlaka ya Usafiri wa Anga inawajulisha wadau wa usafiri wa anga na umma kwa ujumla kwamba Kanuni za Usafiri wa Anga zilizochapishwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 258 hadi 268, la tarehe 18 Septemba 2026, sasa zinapatikana.

Kanuni hizi zinaweka matakwa mapya ya usimamizi na kufanya marekebisho katika matakwa yaliyopo, yakiwemo kuhusu:

a) leseni za wataalamu wa usafiri wa anga na sifa za umahiri;

b) mifumo ya mawasiliano ya urushaji wa droni;

c) usimamizi wa usalama wa usafiri wa anga na ulinzi wa taarifa za usalama;

d) usalama wa usafiri wa anga;

e) usanifu na uendeshaji wa viwanja vya helikopta;

f) matumizi ya masafa ya redio za uongozaji ndege;

g) vigezo vya kubainisha utekelezwaji wa masharti ya usafiri wa anga wa kibiashara;

h) redio za kuongozea ndege;

i) huduma za ndege ardhini; na

j) huduma za hali ya hewa kwa uongozaji ndege.

Waendeshaji, wamiliki wa leseni na vyeti, watoa huduma, wataalamu wa usafiri wa anga na wadau wengine wanaoathirika wanashauriwa kupitia Kanuni hizi na kutathmini athari zake kwa shughuli zao, vibali, miongozo, taratibu, mafunzo, kumbukumbu, mifumo ya usalama, pamoja na mipango ya uzingatiaji wa sheria.

Kanuni hizi pamoja na tangazo la Serikali husika vinapatikana kupitia tovuti rasmi ya Mamlaka, **www.tcaa.go.tz**.

Wadau wanahimizwa kupitia matakwa yanayowahusu na kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha uzingatiaji endelevu wa Kanuni.

**Imetolewa tarehe 21 Septemba 2026.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Mon Sep 21 22:10:26 EAT 2026

Dkt. Jabiri K. Bakari
**Mkurugenzi Mkuu**

Aviation House, Mwisho wa Barabara Nyerere/Kitunda, S.L.P 2819, Dar es Salaam, Tanzania
Email: dg@tcaa.go.tz Telephone: +255-282 560333